

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

CHUO CHA UFUNDI STADI - VETA ULYANKULU

MKATABA WA ZABUNI

Na. ya Mkataba: VETA/ULY/UV20/22/24

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 10 Februari, 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi Veta Ulyankulu S.L.P. 111 Ulyankulu ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

M/S POYONGO GROUP LIMITED (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Uvinza.

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Uvinza;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni kwa ajili ya kuleta Vifaa vya Ujenzi

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Mzabuni Mchanganuo wa Vifaa vya Ujenzi unaoonyesha Vifaa vinavyotakiwa kuletwa;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA ZABUNI

Kwamba, kwa gherama ya Shilingi za Tanzania 1,200,000/= (Millioni Moja Laki Mbili Tu) Mzabuni atafanya kazi hiyo kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

NA.	AINA YA KAZI	KIASI	MAELEZO
1.	VIFAA VYA UJENZI	450,000	
2.	VIFAA VYA UJENZI	750,000	
	JUMLA KUU	1,200,000	

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha Fedha kitajulikana kama "Gharama ya Vifaa vya Ujenzi"

2. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Mzabuni kwa Hundi ndani ya Siku Saba (07) mara baada ya kuleta mzigo

3. MAMBO YALIYO NJE YA UWEZO WA KIBINADAMU

Itakapotokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu kama vile mafuriko, kimbunga, tetemeko la ardhi na mambo yanayofanana na hayo, pande zote mbili zitapata nafasi ya kulijadili na kulipatia ufumbuzi wa haraka.

4. NOTISI (NOTICES)

Mawasiliano yote, Hati, Notisi yatakayofanyika katika Mkataba huu, yatafanyika kwa ama kupelekwa moja kwa moja (physically) kwa upande wowote wa Mkataba au kupitia anwani ya Posta kwa barua iliyosajiliwa (registered mail).

5. SHERIA ZINAZOTUMIKA

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni Sheria za Tanzania.

RUSHWA

6. Iwapo Mzabuni au Wasaidizi wake katika kutekeleza Zabuni hili watajihusisha na masuala yoyote ya Rushwa ama Jinal yoyote, basi Mwajiri anaweza kuvunja Mkataba huu.

KUVUNJWA KWA MKATABA

Mkataba huu unaweza kuvunjwa na upande wowote wa Mkataba huu.

(a) Mkataba kuvunjwa na Mwajiri:

Bila ya kuathiri haki zozote za Mwajiri, Iwapo Mzabuni aktifanya makosa yafuatayo:

- i. Kucheleta kuleta Vifaa kwa wakati bila ya sababu yoyote ya msingi, au
- ii. Kutofuata maelekezo ya Mwajiri wakati wa uletaji wa Vifaa
- iii. Mzabuni akimpa Mtu mwengine kazi ya kuleta Vifaa bila ya kupata Idhini ya Mwajiri

8. USIRI

Nyaraka zote zitakazokuwa zimetumika katika Zabuni inayohusiana na Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa Zabuni inayohusu Mkataba huu. Pia taarifa yoyote itakayopatikana wakati wa Zabuni hili haitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa Zabuni inayohusu Mkataba huu.

9. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhihswa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhihsa mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhihsishi kwa njia ya usuluhihsishi (arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU
NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI CHA
VETA ULYANKULU

Jina: RICHARD MZABUNI

Saini:

R. Mzabuni

Wadhifa: Mzabuni wa Chuo

Tarehe:

10/02/2022

PRINCIPAL VTC ULYANKULU
P.O. ~~Box~~ III
ULYANKULU

Mbele ya (Shahidi)

Jina: JAVARI MATHURIZI Saini:

J. Mathurizi

Wadhifa: MIKTU, KAMATI UTENZI Tarehe:

10/02/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI

Jina:

P. Mzabuni

Saini:

P. Mzabuni

Wadhifa:

Tarehe:

10/02/22

Mbele ya (Shahidi)

Jina:

Sima Hassan

Saini:

S. Hassan

Wadhifa:

Mhd. Hassan

Tarehe:

10.2.2022